4.0 KISWAHILI (102)

4.1 MATOKEO YA MITIHANI WA KISWAHILI

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

Jedwali hili linaonyesha matokeo ya Kiswahili ya miaka ya 2004 hadi 2007.

Jedwali 4: Matokeo ya Kiswahili ya Miaka ya 2004 Hadi 2006.

Mwaka	Karatasi	Watahiniwa	Alama ya Juu	Alama ya Wastani	Alama ya Tanganisho
2004	1		40	16.54	6.67
	2		80	27.78	11.47
	3		80	37.25	13.18
	Jumla	**221,286**	**200**	**81.54**	**26.00**
2005	1		40	20.25	6.37
	2		80	34.08	10.61
	3		80	37.57	14.01
	Jumla	**259,301**	**200**	**91.89**	**26.00**
2006	1		40	15.31	7.68
	2		80	40.60	11.80
	3		80	48.48	14.63
	Jumla	**241,272**	**200**	**104.39**	**29.00**
2007	1		40	15.80	6.42
	2		80	32.22	11.91
	3		80	43.49	13.12
	Jumla	**272,905**	**200**	**91.51**	**27.00**

Jedwali hili laonyesha kuwa:

4.1.1 Alama ya wastani ya karatasi ya 1(102/1) ya mwaka wa 2007 haijabadilika ikilinganishwa na ile ya mwaka wa 2006.

4.1.2 Matokeo ya karatasi ya pili (102/2) ya mwaka wa 2007 yamerudi chini yakilinganishwa na ya mwaka wa 2006.

4.1.3 Vilevile, matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2007 yamerudi chini kutoka alama ***48.48*** mwaka wa 2006 hadi ***43.49*** mwaka wa 2007.

4.1.4 Kushuka kwa karatasi hizi mbili kumeathiri matokeo ya Kiswahili kwa jumla mwaka wa 2007. Alama ya wastani ya Kiswahili ya mwaka wa 2007 imeshuka kutoka ***104.39*** mwaka wa 2006 hadi ***91.51*** mwaka wa 2007.

4.1.5 Alama ya tanganisho inaonyesha kuwa kuna baadhi ya watahiniwa ambao waliweza kujipatia alama nyingi zaidi ya alama ya wastani mwaka wa 2007. Alama hii ilikuwa ***27.00***.

Powered By: www.manyamfranchise.com

4.2 INSHA (102/1)

Jedwali 5: Matokeo ya Karatasi ya Kwanza ya Miaka ya 2004 Hadi 2007

Mwaka	2004	2005	2006	2007
Alama ya wastani	16.54	20.25	15.31	15.80
Alama ya tanganisho	6.67	6.37	7.68	6.42

Jedwali hili laonyesha kwamba isipokuwa mwaka wa 2005, karatasi ya 102/1 imekuwa ikifanywa vibaya na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 20.

Tutachanganua swali la kwanza ambalo lilikuwa la lazima na ambalo halikufanywa vizuri, na vilevile swali la nne ambalo liliwatatiza watahiniwa.

Swali la Kwanza

INSHA YA LAZIMA:
Andika barua kwa mhariri wa gazeti ukilalamikia hali ya watu nchini kwenu kuhamia mataifa ya nje kwa wingi.

Watahiniwa walikosa alama kwa sababu wengi hawakuweza kutofautisha kati ya barua kwa mhariri na makala ya kawaida kwa gazeti. Wengine hawakuweza kufuata muundo wa kuandika barua rasmi ambayo ndiyo ilihitajika. Insha hii ilitakikana iandikwe kama ifuatavyo:

(i) Barua iandikwe kwa muundo wa barua rasmi

- Anwani ya mwandishi juu mkono wa kulia.
- Tarehe chini ya anwani ya mwandishi.
- Anwani ya mhariri upande wa kushoto.
- Mtajo.
- Mada.
- Maudhui.
- Jina la mwandishi laweza kuwa lakabu.
- Sahihi.

(ii) Lugha iakisi malalamiko. Mfano maneno kama ***kera, sikitisha, huzunisha*** n.k yatumiwe.

(iii) Mwili/hoja

- Wanaohama wanavutiwa na maisha mazuri huko nje lakini wengine huisha kuteseka.
- Walioelimika ndio wanaohama kwa wingi. Sekta mbalimbali zinaathirika, kwa mfano: ***matibabu, elimu***, nk.
- Walioelimika wameelimishwa kwa mfuko wa umma. Kuondoka kwao ni hasara kwa nchi.
- Mtu kuhama nchi yake ni kukosa uzalendo.
- Mshikamano wa familia nyingi husika unasambaratika.
- Kuna uwezekano wa kuigiza/kuiga utamaduni wa kigeni.

Swali la Nne

Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Hili lilikuwa swali la methali. Watahiniwa walipotoka katika kutafsiri maana ya methali hiyo wakatoa hoja zilizopotosha. Wengi walielewa methali hii kuwa na maana sawa na ***"mtegemea cha nduguye hufa maskini"***, ambayo ina maana tofauti kabisa.

Majibu yaliyotarajiwa

(a)

- Maana kuwa jambo la mwenzio usilione kuwa lako.
- Kwamba kila mtu ana maisha/sudi yake.
- Usionee mwenzako kijicho.
- Usitegemee mwingine maishani kama msingi wa kujitathmini.

(b) Waandike kisa kuonyesha ukweli wa hali hii, na kama ni ziadi ya kisa kimoja lazima vitegemeane au viwe na muumano/vihusiane.

4.3 MAPENDEKEZO

- Wanafunzi waendelee kupewa mazoezi zaidi ya uandishi wa kiuamilifu.

- Ni vizuri wanafunzi wakisisitiziwa kwamba kuwa na ujuzi wa mambo yanayotokea kila siku huwawezesha kuwa na maoni na hoja za hali ya juu iwapo watatakikana kuandika insha. Kwa hivyo wasome na kujua yanayoendelea katika mazingira yao na hata kitaifa na kimataifa.

4.4 LUGHA (102/2)

Jedwali 6: Matokeo ya Karatasi ya Pili (102/2) ya Miaka ya 2004 Hadi 2007.

Mwaka	**2004**	**2005**	**2006**	**2007**
Alama ya Wastani	27.78	34.08	40.60	32.22
Alama ya Tanganisho	11.47	10.61	11.80	11.91

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yemerudi chini mwaka wa 2007. Matokeo haya yako karibu sawa na yale ya mwaka wa 2005 ambapo alama ya wastani ilikuwa ***34.08***. Maswali ya ufahamu na muhtasari ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa kwa hivyo tutayachanganua hapa.

Swali la 1

Ufahamu

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Takwimu ambazo zimetolewa na shirika la kazi la kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazoukiliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa chachu ya kuumua ari ya maendeleo, elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule kama usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na pashau ya utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

Kwa ujumla, maswali ya kifungu yalihitaji mtahiniwa asome, aelewe na kuchanganua, kusanisi, kutafsiri, kutathmini na kutumia maudhui katika kifungu kujibu maswali. Watahiniwa wengi waliinua majibu moja kwa moja kutoka kwa kifungu, jambo ambalo linafanya majibu yasiwe na mtiririko unaoridhisha. Watahiniwa pia walikosa alama katika swali hili kwa sababu wengi hawana stadi ya kujieleza vizuri na hufanya makosa mengi ya sarufi na tahajia.

Swali la 1 (a)

Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto?

Majibu

Umewafanya wenye nia mbaya kulangua watoto kwa urahisi.

Swali la 1(b)

Mwandishi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto?

Majibu

- Ushirikiano wa kimataifa kuikomesha biashara hii haramu.
- Kuondolewa kwa mfumo fisadi wa kisheria/kuundwa kwa mfumo bora wa kisheria.
- Kuzuia msambaratiko wa muundo wa jamaa.
- Kumaliza ubinafsi wa kijamii.

Swali la 1(c)

Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Majibu

- Kuzongomezwa madanguroni.
- Kufanyishwa kazi za sulubu.
- Kufanyishwa kazi za kitopasi.
- Kuishi maisha duni.

Swali la 1(d)

Kulingana na muktadha, kifungu "chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani?

Majibu

Kichocheo/chanzo/kisababishi/kiini cha kuanzisha/kuhamasisha maendeleo.

Swali la 1(c)

Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani?

Majibu

Kukitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

Swali la 1(f)

(f) Eleza maana ya

(i) maarubu .....

(ii) pashau .....

Majibu

- Lengo/madhumuni/sababu/nia/kusudi/azma/shabaha/kiini/dhamira.
- Tamaa/Shauku/Uchu/Kiu/Hamu.

Swali la pili: Muhtasari

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu katika ulimwengu wa leo. Kimsingi, ubinafsishaji ni hatua na harakati zinazochukuliwa kupunguza kushiriki kwa serikali katika uendeshaji wa mashirika na kuhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.

Serikali huweza kuhimiza, kutokana na uuzaji, uhawilishaji wa mali kutoka umiliki wa umma hadi kwenye umilikaji wa sekta ya kibinafsi. Aidha, serikali inaweza kuuza hisa zake kwenye mashirika ya umma. Njia nyingine ni kuchochea ugavi wa zabuni kupitia kwa mikataba ambayo inashindaniwa na mashirika au kampuni tofauti. Lengo kuu la ubinafsishaji ni kuigatua nafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

Uuzaji wa mashirika ya kiserikali au hisa huwa chanzo cha mapato yanayoweza kutumiwa kuendesha miradi mingine. Hii ni njia ya kupunguza harija ya serikali inayotokana na

Powered By: www.manyamfranchise.com

uendeshaji wa mashirika yasiyoleta faida. Ubinafsishaji huzuia uwezekano wa kuingiliwa kwa mashirika na wanasiasa, huimarisha utamaduni mpya wa muundo wa mashirika na huvunja uhodhi wa kiserikali. Ubinafsishaji huweza kuatika mbegu za ujasiriamali wa raia, kutamani kuanzisha amali tofauti.

Ubinafsishaji huweza kuyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwaa mashirika muhimu nchini, kufutwa kazi kwa wafanyikazi na kuongezeka kwa umaskini. Ubinafsishaji wa sekta zinazohusiana na elimu na afya huweza kuathiri vibaya wenye mapato ya chini.

Ubinafsishaji haumaanishi ufanisi wa utendakazi wa makampuni na mashirika. Aidha, ikiwa haupo utaratibu mzuri wa kutathmini au kupima thamani za hisa pana uwezekano wa hisa zinazouzwa kupewa thamani ya juu au ya chini.

Swali hili lilihitaji mtahiniwa asome kifungu na kusanisi hoja muhimu na kuzifanyia muhtsari bila kuacha mawazo muhimu.

Mtahiniwa pia alihitaji stadi ya kutumia viunganishi vifaavyo ili kuleta mtiririko unaoridhisha. Watahiniwa wengi walilemewa katika upande wa kutumia viunganishi ili kutiririsha mawazo. Wengi waliinua sehemu ambazo hazikuwa na uhusiano wowote kihoja. Stadi ya kujieleza kwa mtiririko ufaao lazima ifundishwe.

Swali la 2(a)

Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya kwanza na ya pili. (maneno 35 - 40)

Matayarisho

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

Majibu

- Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu ulimwenguni.
- Hupunguza kushiriki kwa serikali kuendesha mashirika na huhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.
- Serikali inaweza kuuza hisa kwenye mashirika na kuchochea ugavi wa zabuni.
- Huigatua nafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

Swali la 2(b)

Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya tatu na ya nne.
(maneno 45 - 50)

Matayarisho

.....

.....

Powered By: www.manyamfranchise.com

Nakala safi

.....

.....

Majibu

- Uzaji wa mashirika huletea serikali mapato.
- Huzuia kuingiliwa na wanasiasa.
- Huimarisha utamaduni mpya wa mashirika na kuvunja uhodhi.
- Huweza kuatika ujasiriamali.
- Huyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwaa mashirika muhimu na kufutwa kazi/kuongeza umaskini.
- Ubinafsishaji wa elimu na afya huathiri maskini.
- Si ufanisi wa utendakazi.
- Usipokuwepo, hisa zinazouzwa hushushwa au hupandishwa.

4.5 MAPENDEKEZO

- Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ya maswali ya ufahamu na kusahihisha wakizingatia sarufi kwa sababu jambo hili linazingatiwa wakati wa kusahihisha mtihani wa kitaifa.

- Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi na tathmini kwa hivyo maswali ambayo hayaonekani kuwa na majibu ya kuinua moja kwa moja huulizwa pia.

- Mazoezi ya muhtasari huku mtiririko ufaao ukisisitizwa lazima yapewe wanafunzi mara kwa mara ndio wazoee kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

4.6 FASIHI (102/3)

Jedwali 7: Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2004 hadi 2007.

Mwaka	**2004**	**2005**	**2006**	**2007**
Alama ya Wastani	37.25	37.57	48.48	43.49
Alama ya Tanganisho	13.18	14.01	14.63	13.12

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2007 yameshuka kutoka alama ya wastani ya ***48.48*** mwaka wa 2006 hadi ***43.49*** mwaka wa 2007.

Tutachanganua swali la kwanza pekee katika karatasi hii kwa sababu ndilo lililoonekana kuwapa watahiniwa changamoto kidogo. Swali la ushairi huhitaji mtahiniwa kusoma, kuelewa maudhui ya shairi, dhamira, lugha iliyotumiwa pamoja na istilahi za kifasihi zinazotumiwa. Watahiniwa walitatizika kwa kutozielewa mbinu za kifasihi na pia kushindwa kuandika katika lugha ya nathari ambapo wengi waliinua tu mishororo ya ubeti badala ya kueleza hoja zilizokuwepo kwa lugha ya kawaida.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Swali la 1

(Lazima)
Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:

1 Tohara, usimwazie, mwanamke,
Tohara, usikaribie, mwili wake,
Tohara, usiifikie, ngozi yake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

2 Tohara, hiyo haramu, adha kwake,
Tohara, ni kubwa sumu, si kufu yake,
Tohara, ni za kudumu, dhara zake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

3 Tohara, kile kijembe, usikishike,
Tohara, yule kiumbe, si haki yake,
Tohara, usimtimbe, kwayo makeke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

4 Tohara, ni tamaduni, usiyashike,
Tohara, ati uzimani, ajumuike,
Tohara, umaaluni, kwa mwanamke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

5 Tohara, akijifungua, ataabike,
Tohara, yaweza ua, hufa wanawake,
Tohara, inausumbua, uhai wake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

6 Tohara, na siku hizi, haya uyashike,
Tohara, gonjwa umaizi, lije limshike,
Tohara, ageuke uzi, huo mwili wake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

7 Tohara, nasisitiza, mwanamke,
Tohara, inaibeza, hadhi yake,
Tohara, inadumaza, fikira yake,
Tohara ya mwanamke, zamu yake ipitile!

Swali la 1(a)

Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili.

Majibu

- Si busara/muhimu kumpasha mwanamke tohara.
- Madhara yanatokana na kumpasha mwanamke tohara.

Swali la 1(b)

Fafanua madhara manne ya tohara kwa mwanamke.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Majibu

- Ni sumu.
- Humtimba/kumwumiza.
- Huua.
- Humtaabisha wakati wa kujifungua.
- Hudhalilisha afya.
- Inabeza hadhi yake.
- Inaduwaza fikira.
- Husumbua uhai/maisha.

Swali la 1(c)

Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi.

Majibu

- Jazanda/istiari,
  mf. Tohara ni sumu;
  Ageuke uzi.
- Takriri mf. Tohara/kibwagizo
- Kinaya: kuwa tohara ni utamaduni wa kufanya mtu mzima.
- Chuku: Tohara gonjwa,
  Tohara itaua – ni chuku.
- Tashhisi: Tohara yaweza kuua;
  Tohara hudumaza/sumbua.
- Nidaa/siyahi – katwani siwazie.
- Taswira – ageuke uzi.
- Tasfida – kujifungua.

Swali la 1(d)

Kulingana na mshairi, mwanamke hupashwa tohara kwa nini?

Majibu

- Ati utamaduni unahitaji/ ni mila.
- Ni daraja ya kuingia katika utu uzima.

Swali la 1(e)

Andika ubeti wa sita katika lugha nathari.

Majibu

Inapaswa kufahamu kuwa tohara siku hizi husababisha ugonjwa mbaya ambao huathiri afya ya mwanamke (UKIMWI). Mwanamke hukonda kabisa. Usiwazie hata kidogo kumtahiri mwanamke.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Swali la 1(f)

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi

(i) **adha**
(ii) **usimtimbe**

Majibu

- ***Adha*** – dhiki/masumbuko/shida/madhara.
- ***Usimtimbe*** – usimsumbue/usimtese/usimlazimishe.

Swali la 1(g)

Upashaji wa tohara kwa mwanamke ni mojawapo ya maswala ibuka katika jamii yetu. Taja maswala ibuka mengine mawili yanayohusu mwanamke.

Majibu

- Ndoa za lazima – wasichana.
- Ndoa za mapema kwa watoto wa kike.
- Udhalimu unaoelekezwa wanawake.
- Ubakaji.
- Usawa wa kijinsia.
- Mirathi.
- Unyanyasaji wa kimapenzi.

4.7 MAPENDEKEZO

- Ni vizuri walimu wakiendelea kuonyesha wanafunzi kwamba ushairi ni jambo la kawaida linalowekwa katika lugha ya kishairi ndio waweze kuupenda.

- Walimu wawasaidie wanafunzi kuweza kutofautisha dhamira, maudhui katika ushairi na pia wasaidiwe kutambua mbinu tofauti tofauti za kifasihi katika mashairi.

- Wanafunzi waendelee kusisitiziwa kwamba kuandika katika lugha ya nathari si kuinua mishororo mizima na kuipachika vile ilivyo, bali ni kuitambua hoja muhimu katika kila mshororo na kuiandika.

Powered By: www.manyamfranchise.com

23.2 KISWAHILI (102)

23.2.1 Kiswahili Paper 1(102/1)

102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA
Oct./Nov. 2007
Saa 1 $\frac{3}{4}$

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA
Saa 1 $\frac{3}{4}$

*Andika Insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya lazima.*
Kisha chagua insha moja nyingine kutoka hizo nne zilizobakia.
Kila insha isipungue maneno 400.
Kila insha ina alama 20.

Karatasi hii ina kurasa 2 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

©2007 The Kenya National Examinations Council
Fungua ukurasa

Powered By: www.manyamfranchise.com

1 **INSHA YA LAZIMA:**
Andika barua kwa mhariri wa gazeti ukilalamikia hali ya watu nchini kwenu kuhamia mataifa ya nje kwa wingi.

2 Eleza vile tatizo la uhaba wa maji linavyoweza kutatuliwa hapa nchini.

3 Mshikamano katika familia hutegemea mambo mengi. Fafanua.

4 Bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi.

Powered By: www.manyamfranchise.com

23.2.2 Kiswahili Paper 2(102/2)

Jina ..... **Namba yako** .....

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Oct./Nov. 2007
Saa 2½

Sahihi ya mtahiniwa .....

Tarehe .....

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Saa 2½

Jibu maswali ***yote.***

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA		

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa zawasawa na kuwa maswali yote yamo.

©2007 The Kenya National Examinations Council

Powered By: www.manyamfranchise.com

1 UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Takwimu ambazo zimetolewa na shirika la kazi la kimataifa (ILO) zinaonyesha kuwa ulanguzi wa watoto umetangaa hususan katika mataifa yanayoendelea. Ipo tumbi ya sababu za kuelezea kwa nini biashara hii imeshamiri.

Athari mojawapo ya utandawazi ni kuunda mtandao mpana ulimwenguni. Mtandao huo unaweza kutumiwa kwa njia chanya au njia hasi. Njia chanya ni zile zinazoukiliwa kuwafaidi wanajamii kwa kuendeleza ubinadamu na kuboresha hali ya maisha kiuchumi, kisiasa na kitamaduni. Maarifa yanayosambazwa huweza kuwa chachu ya kuumua ari ya maendeleo, elimu na mafanikio katika mataifa mengi ulimwenguni. Njia hasi ni zile ambazo maarubu yake ni kuwanufaisha wachache huku zikiwahasiri wengi.

Kuwepo kwa mtandao kunawapa wenye nia tule kama usafirishaji na ulanguzi wa watoto fursa ya kuzitosheleza hawaa zao. Wanaoshiriki katika biashara hii huongozwa na pashau ya utajiri. Hawachelei kuwalangua watoto wanaochimbukia mataifa ya kimaskini huko ughaibuni wanakozongomezwa kwenye madanguro, kufanyishwa kazi za sulubu na za kitopasi na kuishi maisha duni.

Asilimia kubwa ya watoto hurubuniwa kwa ahadi ghushi za kujiendeleza kimasomo. Wengine huuzwa kutokana na msaada wa jamaa zao wanaotovukwa na utu na kuwa mawakala katika amali hii ya kusikitisha. Biashara hii huweza kusahilishwa kwa kuwepo kwa mfumo fisadi wa kisheria, msambaratiko wa muundo wa jamaa na ubinafsi wa kijamii.

Ipo haja kubwa ya ushirikiano wa mataifa alkulihali kuikomesha biashara hii haramu. Jamii ya ulimwengu isipofanya hivi, itakuwa imekitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri.

(a) Ni kwa jinsi gani utandawazi umechangia katika biashara ya ulanguzi wa watoto? (alama 2)

(b) Mwandishi wa kifungu anapendekeza hatua zipi kusuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto?

(c) Eleza jinsi watoto wanaolanguliwa wanavyoishi huko ughaibuni. (alama 3)

(d) Kulingana na muktadha, kifungu "chachu ya kuumua ari ya maendeleo" kina maana gani? (alama 2)

(e) Jamii isiyosuluhisha tatizo la ulanguzi wa watoto itakuwa na hatima gani? (alama 3)

(f) Eleza maana ya

(i) maarubu .....

(ii) pashau .....

(alama 2)

Powered By: www.manyamfranchise.com

2 MUHTASARI

Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu katika ulimwengu wa leo. Kimsingi, ubinafsishaji ni hatua na harakati zinazochukuliwa kupunguza kushiriki kwa serikali katika uendeshaji wa mashirika na kuhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.

Serikali huweza kuhimiza, kutokana na uuzaji, uhawilishaji wa mali kutoka umiliki wa umma hadi kwenye umilikaji wa sekta ya kibinafsi. Aidha, serikali inaweza kuuza hisa zake kwenye mashirika ya umma. Njia nyingine ni kuchochea ugavi wa zabuni kupitia kwa mikataba ambayo inashindaniwa na mashirika au kampuni tofauti. Lengo kuu la ubinafsishaji ni kuigatua nafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

Uuzaji wa mashirika ya kiserikali au hisa huwa chanzo cha mapato yanayoweza kutumiwa kuendesha miradi mingine. Hii ni njia ya kupunguza harija ya serikali inayotokana na uendeshaji wa mashirika yasiyoleta faida. Ubinafsishaji huzuia uwezekano wa kuingiliwa kwa mashirika na wanasiasa, huimarisha utamaduni mpya wa muundo wa mashirika na huvunja uhodhi wa kiserikali. Ubinafsishaji huweza kuatika mbegu za ujasiriamali wa raia, kutamani kuanzisha amali tofauti.

Ubinafsishaji huweza kuyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwaa mashirika muhimu nchini, kufutwa kazi kwa wafanyikazi na kuongezeka kwa umaskini. Ubinafsishaji wa sekta zinazohusiana na elimu na afya huweza kuathiri vibaya wenye mapato ya chini.

Ubinafsishaji haumaanishi ufanisi wa utendakazi wa makampuni na mashirika. Aidha, ikiwa haupo utaratibu mzuri wa kutathmini au kupima thamani za hisa pana uwezekano wa hisa zinazouzwa kupewa thamani ya juu au ya chini.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa kifungu, fanya muhtasari wa aya ya kwanza na ya pili. (maneno 35 - 40) (alama 6, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya tatu na ya nne.
(maneno 45 - 50) alama 9, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

3 MATUMIZI YA LUGHA

(a) Tunga sentensi moja ukitumia nomino dhahania. (alama 2)

(b) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo:

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Nzovu na Bi Makambo. (alama 2)

(c) Unda nomino moja kutokana na kitenzi "ghafilika". (alama 1)

(d) Andika kwa wingi: Nyundo hii imevunjika mpini wake. (alama 1)

(e) Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia jedwali.

Mvulana mrefu anavuka barabara. (alama 3)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(f) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo. (alama 2)

(i) Karama .....

(ii) Gharama .....

(g) Tambua na ueleze aina za vivumishi katika sentensi zifuatazo:

(i) Mtoto mwenyewe alienda shambani. (alama 1)

(ii) Kazi yetu haihitajiki shuleni. (alama 1)

(h) Koloni/nukta mbili (:) hutumiwa katika kuorodhesha. Onyesha matumizi mengine matatu ya koloni (:) (alama 3)

(i) Tunga sentensi itakayoonyesha matumizi ya kihusishi cha a-unganifu. (alama 2)

(j) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo 'Mkulima aliyepanda wakati ufaao amepata mavuno mazuri.' (alama 2)

(k) Ainisha viambishi katika neno: **kujidhiki.** (alama 2)

(l) Tambua na ueleze aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo
'Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.' (alama 2)

(m) Andika viwakilishi ngeli vya nomino zifuatazo:

(i) Chakula ..... (alama 1)

(ii) Kwetu ..... (alama 1)

(n) Badilisha sentensi ifuatayo ili iwe katika hali ya kuamuru.
Baba ingia ndani. (alama 2)

(o) Eleza maana ya sentensi
'Ningalikuwa na pesa ningalinunua nyumba na ningalistarehe'. (alama 2)

(p) Fafanua aina za hali zinazotumika katika sentensi hizi.

(i) Mwimbaji aliimba, akacheza na akachanganisha sana. (alama 1)

(ii) Shangazi huja kila mara. (alama 1)

(q) Tunga sentensi MOJA itakayoonyesha maana mbili tofauti za neno **pembe.** (alama 2)

(r) Andika katika msemo wa taarifa "Nitakuarifu nikimwona", Elma alisema. (alama 3)

.....

(s) Nyambua kitenzi "ota" kama kinavyotokea katika kirai "ota ndoto" ili tofauti tatu zijitokeze. (alama 3)

4. Isimu Jamii

Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua kaida tano katika jamii ambazo matumizi ya lugha hutegemea. (alama 10)

Powered By: www.manyamfranchise.com

23.2.3 Kiswahili Paper 3(102/3)

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI YA KISWAHILI
Oct./Nov. 2007
Saa: $2^1/_2$

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI YA KISWAHILI
Saa: $2^1/_2$

Jibu maswali manne pekee.
Swali la kwanza ni la ***lazima.***
Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.
Usijibu maswali ***mawili*** *kutoka katika* ***sehemu moja.***

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

7015

© *2007 The Kenya National Examinations Council*

Fungua ukurasa

Powered By: www.manyamfranchise.com

1 (Lazima)

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata:

1 Tohara, usimwazie, mwanamke,
Tohara, usikaribie, mwili wake,
Tohara, usiifikie, ngozi yake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

2 Tohara, hiyo haramu, adha kwake,
Tohara, ni kubwa sumu, si kufu yake,
Tohara, ni za kudumu, dhara zake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

3 Tohara, kile kijembe, usikishike,
Tohara, yule kiumbe, si haki yake,
Tohara, usimtimbe, kwayo makeke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

4 Tohara, ni tamaduni, usiyashike,
Tohara, ati uzimani, ajumuike,
Tohara, umaaluni, kwa mwanamke,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

5 Tohara, akijifungua, ataabike,
Tohara, yaweza ua, hufa wanawake,
Tohara, inausumbua, uhai wake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

6 Tohara, na siku hizi, haya uyashike,
Tohara, gonjwa umaizi, lije limshike,
Tohara, ageuke uzi, huo mwili wake,
Tohara ya mwanamke, katwaani siwazie!

7 Tohara, nasisitiza, mwanamke,
Tohara, inaibeza, hadhi yake,
Tohara, inadumaza, fikira yake,
Tohara ya mwanamke, zamu yake ipitile!

(a) Eleza dhamira ya msanii katika shairi hili. (alama 2)

(b) Fafanua madhara manne ya tohara kwa mwanamke. (alama 4)

(c) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi. (alama 4)

(d) Kulingana na mshairi, mwanamke hupashwa tohara kwa nini? (alama 2)

(e) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi

(i) adha
(ii) usimtimbe

(alama 2)

(g) Upashaji wa tohara kwa mwanamke ni mojawapo ya maswala ibuka katika jamii yetu. Taja maswala ibuka mengine mawili yanayohusu mwanamke.
(alama 2)

RIWAYA

Z. BURHANI: *Mwisho wa Kosa*

Jibu swali la 2 au la 3

2 Onyesha jinsi ukengeushi unavyojitokeza katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. (alama 20)

3 Eleza jinsi ambavyo KINAYA kimetumiwa katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*. (alama 20)

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: *Kifo Kisimani*

Jibu swali la 4 au la 5.

4 Ukirejelea tamthilia ya *Kifo Kisimani*, fafanua mambo yanayopiganiwa na umma katika nchi ya Butangi. (alama 20)

5 "Uovu wa mume si uovu wa *mke*"

(a) Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi mhusika anayerejelewa hapa alivyosaidia kupunguza mateso ya wana Butangi. (alama 10)

(c) Eleza wasifu wa msemaji. (alama 6)

Powered By: www.manyamfranchise.com

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA: *Mayai Waziri wa Maradhi*

6 "Mimi nashughulika na wanyama wa porini, mambo yanayohusu binadamu mimi simo".

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

(b) Onyesha jinsi mzungumzaji na wenzake wasivyowajali wananchi wanaowahudumia. (alama 16)

FASIHI SIMULIZI

7 (a) Nini maana ya mighani/migani? (alama 4)

(b) Fafanua sifa tano za mighani/migani. (alama 10)

(c) Eleza umuhimu wa mighani/migani. (alama 6)

Powered By: www.manyamfranchise.com

24.2 KISWAHILI (102)

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

24.2.1 Kiswahili Karatasi ya 1 (102/1)

Swali la Kwanza

(a) Barua iandikwe kwa muundo wa barua rasmi

- Anwani ya mwandishi juu mkono wa kulia.
- Tarehe chini ya anwani ya mwandishi.
- Anwani ya mhariri upande wa kushoto.
- Mtajo.
- Mada.
- Maudhui.
- Jina la mwandishi laweza kuwa lakabu.
- Sahihi.

(b) Lugha iakisi malalamiko. Mfano maneno kama kera, udhi, sikitisha, huzunisha nk yatumiwe.

(c) Mwili/hoja

- Wanaohama wanavutiwa na maisha mazuri huko nje lakini huishia kuteseka.
- Walioelimika ndio wanaohama kwa wingi. Sekta mbalimbali zinaathirika mf matibabu, elimu, nk.
- Walioelimika wameelimishwa kwa mfuko wa umma. Kuondoka kwao ni hasara kwa nchi.
- Mtu kuhama nchi yake ni kukosa uzalendo.
- Mshikamano wa familia nyingi husika unasambaratika.
- Kuna uwezekano wa kuigiza/kuiga utamaduni wa kigeni. ***(Alama 20)***

Swali la Pili

- Kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi bora ya maji.
- Umuhimu wa kuhifadhi na kutochafua maji.
- Kuhifadhi chemichemi zote za maji ili zisije kukauka.
- Kuchimba visima zaidi hasa katika sehemu kame.
- Kutafuta njia za kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua ili yatumike vyema.
- Kufanya utafiti kuhusu namna ya kubadilisha maji ya chumvi ili yaweze kutumika manyumbani na pia viwandani na mashambani.
- Kupanda miti ya kienyeji ambayo itasaidia kuhifadhi chemichemi za maji.
- Kuzuia watu kujenga karibu na vyanzo vya maji.
- Kuhimiza umma kutumia maji kwa uangalifu bila kuyaharibu.
- Kutafuta njia ambapo maji taka na mengine yaliyotumika yanaweza yakasafishwa na kutumika tena.
- Kuwepo kwa sheria kali za kuzuia uhodhi wa maji na yeyote yule.
- Kujengwa kwa mabwawa hasa katika sehemu kame nchini. ***(Alama 20)***

Swali la Tatu

Mshikamano ni hali ya watu kuwa na msimamo mmoja na ushirikiano wa karibu katika kutimiza azma Fulani. Hutegemea

- Mawasiliano.
- Ukweli.
- Ushauri na nasaha.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Bidii kazini kwa kila mwana familia.
- Kukiri makosa.
- Subira.
- Mapenzi.
- Uaminifu.
- Uwajibikaji.
- Kutegemeana na kusaidiana.
- Kuweka malengo ya kuafikiwa na wanafamilia wote.
- Walezi kuwa vielelezo. ***(Alama 20)***

Swali la Nne

(a)

- Maana kuwa jambo la mwenzio usilione kuwa lako.
- Kwamba kila mtu ana maisha/sudi yake.
- Usionee mwenzako kijicho.
- Usitegemee mwingine maishani kama msingi wa Kujitathmini.

(b) Waandike kisa kuonyesha ukweli wa hali hii. Kama ni zaidi ya kisa kimoja lazima vitegemeane au viwe na muumano. ***(Alama 20)***

24.2.2 Kiswahili Karatasi ya 2 (102/2)

Swali la Kwanza

(a) Umewafanya wenye nia mbaya kulangua watoto kwa urahisi. ***(Alama 2)***

(b) (i) Ushirikiano wa kimataifa kuikomesha biashara hii haramu.
(ii) Kuondolewa kwa mfumo fisadi wa kisheria/kuundwa kwa mfumo bora wa kisheria.
(iii) Kuzuia msambaratiko wa muundo wa jamaa.
(iv) Kumaliza ubinafsi wa kijamii. ***(Zozote 3 x 1 = Alama 3)***

(c) (i) Kuzongomezwa mandaguroni.
(ii) Kufanyishwa kazi za sulubu.
(iii) Kufanyishwa kazi za kitopasi.
(iv) Kuishi maisha duni. ***(Alama3)***

(d) Kichocheo/chanzo/kisababishi/kiini cha kuanzisha/kuhamasisha maendeleo. ***(Alama 2)***

(e) Kukitia kizazi kizima kitanzi na kuitumbukiza kesho yake kwenye matatizo kathiri. ***(Alama 3)***

(f) (i) Lengo/madhumuni/sababu/nia/kusudi/azma/shabaha/kiini/dhamira. ***(Alama 1)***
(ii) Tamaa/Shauku/Uchu/Kiu/hamu. ***(Alama 1)***

Swali la Pili

(a)

- Ubinafsishaji wa mashirika ya umma ni nguzo kuu ulimwenguni.
- Hupunguza kushiriki kwa serikali kuendesha mashirika na huhimiza kupanuka kwa sekta ya kibinafsi.
- Serikali inaweza kuuza hisa kwenye mashirika na kuchochea ugavi wa zabuni.
- Hugatua nafasi ya serikali katika utendakazi na uendeshaji wa mashirika.

(Alama 6)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(b)

- Uzaji wa mashirika huletea serikali mapato.
- Huzuia kuingiliwa na wanasiasa.
- Huimarisha utamaduni mpya wa mashirika na kuvunja uhodhia.
- Huweza kuatika ujasiriamali.
- Huyaruhusu mashirika ya kimataifa kutwa mashirika muhimu na kufutwa kazi/kuongeza umaskini.
- Ubinafsishaji wa elimu na afya huathiri maskini.
- Si ufanisi wa utendakazi.
- Usipokuwepo, hisa zinazouzwa hushushwa au hupandishwa. ***(Alama 9)***

Swali la Tatu

a) Mifano ya nomino dhahania: Ubaya, ujinga, uzembe, uvivu, chuki, wema, urembo, ushetani n.k
K.m. – Ubaya wake ulimletea matatizo. ***(Alama 2)***

b) (i) Watoto hawa wote ni wa Bwana Nzovu na Bi. Makambo.
(ii) Baadhi ya watoto hawa ni wa marehemu Bi. Nzovu ilhali wengine ni wa marehemu Bi. Makambo.
(iii) Marehemu ni. Bw. Nzovu pekee.
(iv) Wote wawili, Bw. Nzovu na Bi. Makambo ni marehemu.
(v) Wakati wa kuwajulisha – Yaani hawa ni watoto wa Bw. Nzovu ambaye ni marehemu na wako pamoja na Bi. Makambo.
(vi) Watoto hawa ni mayatima. ***(Zozote 2 x 1 = Alama 2)***

c) Kughafilika, ghafiliko, kighafilishi, mghafilishi, mghafilikiwa, ughafili, mgafilikishi, mghafilikiwa, mghafilika, ughafilishwaji, mghafilika, ughafilikaji, mgafilishwa, ghafili, mgafiliswaji. ***(Alama 1)***

d) Nyundo hizi zimevunjika mipini yao. ***(Alama 1)***

e)

S			
KN		KT	
N	V	T	KN
			N
Mvulana	Mrefu	anavuka	barabara

au

S			
KN		KT	
N	V	T	KN
			N/E
Mvulana	Mrefu	anavuka	barabara

(Alama 3)

f) (i) Karama – Kipawa au uwezo kutoka kwa Mungu/buruhani.
Sentensi – Juma ana karama ya kuombea wagonjwa wakapona. ***(Alama 1)***

(ii) Gharama – Kinachotolewa, hasa pesa, kulipia vitu; matumizi makubwa ya pesa.
Sentensi – Gharama ya maisha imepanda sana siku hizi. ***(Alama 1)***

g) (i) Mwenyewe - Kivumishi cha pekee.
(ii) Yetu - Kivumishi kimilikishi. ***(Alama 2)***

Powered By: www.manyamfranchise.com

h) (i) Kuonyeshea saa.
(ii) Kuonyeshea mafungu ya Bibilia au msahafu.
(iii) Kuonyeshea tarehe.
(iv) Kuandika mada.
(v) Kuonyeshea maneno ya msemaji katika tamthilia/mahojiano/Dayolojia.
(vi) Katika maandishi wakati wa kunukuu kifungu.
(vii) Katika uiano K.M. 1:3.
(viii) Kuandika barua rasmi K.M Kuhusu: Maombi ya Kazi.
(ix) Kuandika wasifu kazi /tawasifu.
(x) Kuandika ufafanuzi – K.M. Mkoa : Nairobi , Wilaya: Kamukunji.
(xi) Kuandika mdahalishi K.M. Barua pepe au kipepesi.
(xii) Kuandika ratiba K.M. Ratiba ya arusi au mazishi. ***(Zozote 3 x 1 = Alama 3)***

i) Mifano ya vihusishi vya a – unganifu
La, wa, cha, vya, kwa, za n.k
K.M Kitabu cha mwanafunzi kimepotea. ***(Alama 2)***

j) (i) Kishazi tegemezi - Mkulima aliyepanda wakati ufaao ***AU***
- aliyepanda wakati ufaao.
(ii) Kishazi huru - Mkulima amepata mavuno mazuri ***AU***
- amepata mavuno mazuri. ***(Alama 2)***

k) Ku - kiambishi cha ngeli/kitenzi jina. ***(Alama 1)***
Ji - kiambishi cha kujirejelea/kirejeshi/mtenda/mtendaji/yambwa (shamirisho).
(Alama 2)

l) (i) aliyokuwa-kitenzi kishirikishi kikamilifu.
(ii) ni - kitenzi kishirikishi kipungufu. ***(Alama 2)***

m) (i) Ki (ki-vi) ***(Alama 1)***
(ii) Ku (ku-ku) ***(Alama 1)***

n)
- Baba ingia ndani!
- Baba, ingia ndani.
- Baba! Ingia ndani.
- Ingia ndani baba! ***(1 x 2 = Alama 2)***

o) Hakuwa na pesa, hakununua nyumba na hakustarehe.
AU
Wakati uliopita.
AU
Hakuna *Uwezekano.*
AU
Hakuna matumaini. ***(Alama 2)***

p) (i) Mfululizo wa matukio. ***(Alama 1)***
(ii) Mazoea. ***(Alama 1)***

q)
- Pembe.
- Kiungo cha mnyama.
- Ukingo/kingo za kitu au eneo K.M. pembe za nchi, pembe za dunia.
- Ncha za vitu zinapokutania.
- Faragha au mahali pa siri.
- Baragumu k.m Mnyama mwenye pembe aligonga kwenye pembe ya nyumba
(Alama 2)

Powered By: www.manyamfranchise.com

r) Elma alisema (kuwa/kwamba) angemwarifu (endapo/ikiwa/kama/iwapo) angemwona. ***(Alama 3)***

s)

- Otesha ndoto.
- Oteshwa ndoto.
- Oteshana ndoto.
- Otea ndoto.
- Otewa ndoto. ***(Zozote 3 x 1 = Alama 3)***

Swali la Nne

- Cheo/hadhi.
- Umri.
- Mada.
- Mazingira/mahali.
- Jinsia/Uana.
- Elimu (kiwango).
- Hali/hisia.
- Muktadha.
- Lugha azijuazo mtu.
- Wahusika.
- Wakati/misimu.
- Uhusiano.
- Mudhumuni/Lengo.
- Malezi.
- Tabaka.
- Taaluma.
- Njia ya mawasiliano. ***(Zozote 5 x 2 = Alama 10)***

Mfano wa Jibu

Umri- Watu wa umri mdogo hutumia lugha ya kutaniana, isiyo sanifu na yenye porojo tele ilhali watu wa umri mkubwa hutumia lugha fasaha na yenye heshima.

24.2.3 Kiswahili Karatasi ya 3 (102/3)

Swali la Kwanza

(a) Si busara/muhimu kumpasha mwanamke tohara- madhara yanayotokana na kumpasha mwanamke tohara. ***(Alama 2)***

(b)

- Ni sumu.
- Humtimba/kumwumiza.
- Huua.
- Humtaabisha wakati wa kujifungua.
- Hudhalilisha afya.
- Inabeza hadhi yake.
- Inadumaza fikira. ***(Zozote 4 x 1 = Alama 4)***

(c) (i) Jazanda

Tohara ni sumu.
Ageuke uzi.

(ii) Takriri.
(iii) Kinaya: kuwa tohara ni utamaduni wa kufanya mtu mzima.
(iv) Chuku: Tohara gonjwa.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Tohara itaua – ni chuku.

(v) Tashhisi: Tohara usiharibu.
Mwili wake.

(vi) Mdokezo:Gonjwa (la UKIMWI)/kukonda. ***(Zozote 2 x 2 = Alama 4)***

(d)

- Ati utamaduni unahitaji/ni mila.
- Ni daraja ya kuingia katika utu uzima. ***(Alama 2)***

(e) Inapaswa kufahamu kuwa tohara siku hizi husababisha ugonjwa mbaya ambao huathiri afya ya mwanamke (UKIMWI). Mwanamke hukonda kabisa. Usiwazie hata kidogo kumtahiri mwanamke. ***(Alama 4)***

(f) (i) Adha – dhiki/masumbuko.
(ii) Usimtimbe – usimsumbue . ***(Alama 2)***

(g)

- Ndoa za lazima – kwa wasichana.
- Ndoa za mapema kwa watoto wa kike.
- Udhalimu unaoelekezwa wanawake. ***(Zozote 2 x 1 = Alama 2)***

Swali la Pili

- Kiburi na majivuno ya wenye elimu na vyeo mfano Monika kupuuza watu waliokuja kumlaki katika uwanja wa ndege.
- Wengi wanavutiwa na mambo ya kigeni na kupuuza ya kwao.
- Wananchi kutothamini bidhaa zinazozalishwa nchini.
- Vijana wengi waliosoma hawana heshima kwa wazazi na wazee.
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya na sigara.
- Utegemezi na kuwatumikia wengine kwa manufaa binafsi.
- Vijana kuathiriwa na utamaduni wa nje hasa mavazi, miziki, mienendo nk.
- Ubinafsi
- Kusifu mambo ya kigeni na tabia za uzunguni.
- Uasi wa desturi za jamii hasa ndoa za kupanga.
- Kupenda starehe nyingi.
- Desturi za kigeni kama Rashid kuishi na Monica kabla ya kumuoa.

(Zozote 10 x 2 = Alama 20)

Swali la Tatu

Kinaya: Tamathali/mbinu ambapo pana mgongano baina ya kile kisemwacho na hali halisi/ukweli wenyewe , mgongano kati ya mazungumzo/matendo na hali yenyewe/kinyume cha mambo.

Mifano:

- Monika anapokelewa na wanakijiji kwa bashasha kwenye uwanja wa ndege lakini mwenyewe anawapuuza.
- Mamake Monika kulazimika kwenda kumkopa Salama pesa ilhali Monika anafanya kazi/mshahara wake ni mkubwa.
- Bi keti anajitolea kama jirani kupeana uji apelekewe Monika ambaye anautupa kwa kudharau.
- Monika kutorokea mjini kwa kuwa hataki kutoa msaada kwa jamaa zake na kukutana na wajanja wanaomzidi maarifa.
- Monika kudharau ndoa za kupangwa na kuishia kuozwa mwenyewe.
- Monika kutarajia kuolewa na Matata ilhali Matata amepanga kuoa msichana mwingine.
- Muna ambaye ameelimika sana anaishia kuishi maisha ya ndoa yenye dhiki na mtu anayedharau elimu hiyo.
- Monika kufurahi kuwa amefahamiana na "waziri" Juma ilhali mwenyewe ni dereva tu.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Jamaa ya Monika ya kimaskini kujitolea kumsomesha naye kwenda kinyume na matarajio.
- Monika kutoroka nyumbani kwa kiburi na kupunjwa na kuenda kutafuta msaada wa waziri Selemani.
- Monika ana elimu ya juu; wenye elimu ya chini kama Salama wanamshinda akili.
- Rashid kusoma barua ya kufutwa kazi na "kucheka kwa uchungu".(u.k. 204)
- Waziri wa Fedha kumfuta Rashid kazi badaaye waziri mwenyewe anajuta kutokana na kitendo hicho. ***(Zozote 10 x 2 = Alama 20)***

Swali la Nne

- Kudumisha haki za kibinadamu.
- Kupinga udunishaji wa wanawake.
- Kuondoa ujinga.
- Kupinga uongozi mbaya.
- Kupinga udanganyifu na unafiki.
- Kupinga uharibifu wa mazingira.
- Kupinga unyakuzi wa ardhi.
- Kupinga maonevu na mateso.
- Kupinga ubaguzi na mapendeleo.
- Kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe.
- Kupinga mauaji na umwagikaji wa damu.
- Kudunisha haki za wafungwa.
- Vita dhidi ya njaa na umaskini.
- Vita dhidi ya ubarakala.
- Kupigana kutafuta mabadiliko ya kuwafaa raia. ***(Zozote 10 x 2 = Alama 20)***

Swali la 5

(a) Mapinduzi ya umma yanatokea. Mtemi na vibaraka wake wanashikwa. Baada ya Andua kumfunga Bokono mikono, Atega anamsihi asimfunge Nyalwe pia kwa sababu hakuwa mwovu kama mumewe. ***(Alama 4)***

(b)

- Alimsimanga Mtemi kwa kuogopa kuondolewa mamlakani.
- Alimshauri mtemi abadili mienendo yake mibaya kama uongozi mbaya.
- Alimtaka mumewe aache kutenda mambo yaliyowaumiza watawaliwa.
- Alionya juu ya udanganyifu na unafiki wa washauri wa Mtemi.
- Alimnasihi Mtemi atende mambo ya kiutu uzima.
- Aliwasilisha kwa Mtemi malalamiko ya wananchi.
- Alimkumbusha Mtemi umuhimu wa kuzingatia kanuni za utawala.
- Alimkejeli mumewe kwa kupenda kusikiza sifa za uongo.
- Aliwakaribisha raia kwake kutoa malalamiko.
- Alimkaripia mumewe kwa kuidhinisha ugawaji wa ardhi ya umma kwa vibaraka wake.

(10 x 1 = Alama 10)

(c)

- Alitaka Mwelusi aachiliwe kutoka kifungoni.
- Alikuwa mwenye utu/ubinadamu.
- Ni mtetezi wa haki.
- Hakati tamaa.
- Ni mwanamapinduzi.
- Ni mwenye akili tambuzi. ***(6 x 1 = Alama6)***

Powered By: www.manyamfranchise.com

Swali la Sita

(a) Mayai Waziri wa Maradhi baada ya kushuhudia mazimwi ya watoto nyumbani kwake akiongozwa na marehemu mwanawake Mkombozi anapiga simu kwa Balozi wa Nyumba Kumi ambaye pia ni waziri wa wanyama pori kutafuta usaidizi. Hili ndilo jibu alilopata waziri.

(Alama 4)

(b)

- Hawaangalii maslahi ya raia.
- Hawazingatii ushauri wa wananchi.
- Wanapenda na kutukuza mambo kutoka nchi za nje.
- Wanadharau kazi wanazoziona duni kama vile ualimu.
- Wanafanya njama na majangiri na watu wanaohujumu maendeleo.
- Wao wana shibe huku umma una njaa.
- Wanaishi kwenye maeneo ya kifahari lakini maskini wanateseka.
- Wanawatumia wananchi kutumbuiza na kutoa sifa wasizostahili.
- Wanawacheka wakulima.
- Wanakwepa majukumu na kutegea kazi
- Wanatoa ahadi za uongo.
- Sera na mipango yao haiwanufaishi wananchi.
- Sera haziwafaidi raia.
- Hawajui matatizo yanayowakabili wananchi. ***(Zozote 8 x 2 = Alama 16)***

Swali la Saba

(a)

- Hadithi/ngano za mashujaa.
- Ni hadithi zinazosimulia mambo ya kishujaa.
- Wanaosimuliwa huwa ni mtu au watu.
- Wanaotukuzwa kwa ushujaa wao uliofaidi jamii. Mf, Mekatilili, Lwanda Magere, Syokimau, Wangu wa Makeri, Koitalel Arap Samoei, Kenyatta, Nyerere nk. ***(Zozote 4 x 1 = Alama 4)***

(b) Mashujaa wanaosimuliwa huwa na sifa kama vile:

- Wana maumbile yasiyo ya kawaida km Fumo Liyongo.
- Kuzaliwa kwa baadhi si kwa kawaida.
- Umbo angalau huwa ni pandikizi la mtu au kidudu mtu.
- Huwa na uwezo wa kutenda mambo ya kuajabia ambayo mtu wa kawaida hawezi kutenda.
- Aghalabu hawafi au kuulika kwa urahisi isipokuwa wanaposalitiwa.
- Mara nyingi mashujaa hawa hujitoa mhanga kutetea umma hasa wanaonyanyaswa.
- Matumizi ya chuku katika utambaji.
- Vifo vyao huingiza jamii katika shida.
- Matumizi ya nyimbo katika utambaji wa mighani. ***(Zozote 5 x 2 =Alama 10)***

(c)

- Ni njia moja ya kupitisha/kufunza historia ya jamii.
- Hufunza maadili.
- Kutukuza matendo ya kishujaa.
- Kukuza ujasiri na ukakamavu miongoni mwa wanajamii.
- Huburudisha.
- Huelimisha wanajamii kuhusu maisha.
- Hufunza utamaduni wa jamii. ***(Zozote 6 x 1 = Alama 6)***

Powered By: www.manyamfranchise.com